

MWANAFUNZI WA BIBILIA - 9 Msamaha



Utangulizi

Kibinadamu, msamaha hujengea maana ya kwamba hakuna tena hasira ama ukakasi juu ya kosa lililofanyika. Pia kuondoa ama kuachilia deni ambalo mtu anadaiwa. Maana kubwa kabisa ya msamaha katika bibilia ina maana ya hali ya mwenye dhambi kutengwa mbali na dhambi zake. Hali hii inaingia kwa undani kuliko ambavyo mawazo ya mwanadamu yanaweza kufikiri. Kimsingi, maana ya msamaha ni ya kwamba mtu ambaye amekosewa anaamua kutokumhesabia hatia mkosaji, na hatampa adhabu yoyote kwa ajili ya kosa hilo. Kosa hilo linaweza likawa ni dhambi dhidi ya Mungu ama dhidi ya kumtendea mwanadamu (ama vyote viwili, mfano kama ni kuu ambapo kwa uhakika ni kosa dhidi ya muathirika na pia ni kosa dhidi ya sheria ya Mungu). Tunaposhindwa kumpenda muumba – ama kutokutii sheria zake – ni kutenda dhambi dhidi yake, na kwahiyo ni jambo linalohitaji msamaha.

Mungu anaposamehe dhambi kuna hali ya unafuu kwa mzigo ambao mtu ameubeba. Juu ya yote, ina maana kwamba adhabu dhidi ya ile dhambi iliyotendwa haihitaji tena kulipwa na yule aliyetenda dhambi. Msamaha haumaanishi kwamba ile dhambi (iliyosamehewa) haina madhara katika ulimwengu huu – jambo la kusikitisha ni kwamba madhara yake yanaweza kuendelea kuonekana. Neno la Kiyunani katika Agano Jipya lenye kumaanisha ‘msamaha’ ni ‘aphiemi’ (kuondoa). Kama tulivyoona katika somo letu la 7, mwenye dhambi aliyesamehewa ‘anahesabiwa haki’ mbele za Mungu. Yule aliyesamehewa anaweza kusema, ‘Ni kama vile sijawahi kutenda dhambi hata mara moja’. Ni dhahiri ya kwamba tabia za dhambi zinapaswa kuachwa kabisa. Yesu alimuambia mwenye dhambi aliyesamehewa, ‘... nenda usitende dhambi tena’ (Yohana 8:11b) Mwenye dhambi aliyesamehewa anapaswa kuwa na hekima na kuepuka mazingira yanayoweza kumtia majaribuni katika siku za usoni, na hasa kama kuna kile kitiwacho ‘dhambi inayomnyemelea’.

Agano la Kale

Je ni nani anayeweza kusamehewa? Katika Agano la Kale, mtu yeyote aliye mwanaume ama mwanamke, anayetubu dhambi zake kwa kweli (ikiwa ni pamoja na toba na kulipa fidia mahali ambapo dhambi ilitendwa dhidi ya mtu mwingine) anaweza kupewa msamaha. Mara nyingi kafara ya damu kwa kadiri ya sheria (Torati) iliweza kufanywa, na ambapo msamaha uliweza kutolewa na Mungu. Hata hivyo ‘damu ya ng’ombe na mbuzi haiwezi kuondoa dhambi’. Kafara katika Agano la Kale ilikuwa ni kwaajili ya kututazamisha kafara iliyo kuu zaidi (ya mwisho) ambayo siku moja ingefanywa na Bwana Yesu. Tazama Mambo ya Walawi 4:20, 26, 5:10, 18 (maelezo ya undani juu ya sadaka ya dhambi yanahitajika); Hesabu 15: 25-26 (makuhani waliweza kutoa kafara kwaajili ya jamii) Zaburi 32:5; 66:18; 103:12 (umuhimu ulikuwepo wa kuachana na kutubu dhambi ulisisitizwa); Isaya 44:22 (Mungu aliwaokoa watu wake, aliondolea mbali makosa yao na aliwaita wamgeukie yeye). Katika Yeremia 31:33-34 tunaonyeshwa ya kwamba wakati unakuja ambapo sheria ya Mungu itaandikwa katika mioyo ya watu wake na kwamba watamfahamu kipekee, na kufahamu msamaha wake.

Agano Jipya

Kafara za Agano la Kale zinakamilishwa na Yesu (Tazama Waebrania 9:22–28) Yesu alisema, ‘Hii ni damu yangu ya Agano Jipya, iliyomwagika kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi’ (Mathayo 26:28) Pia tazama Mathayo 9:2, 5-6. Huu ni uthibitisho wa huduma ya Yesu ya kuondoa dhambi za ulimwengu (Yohana 1:29). Hata hivyo, ni muhimu kukumbuka ya kwamba, Yesu huondoa dhambi za wale tu wanaotubu kwa kweli. Dhambi za wasio tubu hubakia palepale.

Msamaha ni kwa neema ya Mungu

Umuhimu wa neema ni kwamba msamaha unatolewa kama zawadi inayotolewa bure (yaani Kristo amekwisha kulipa adhabu ya dhambi, alipokufa ili sisi tuweze kuishi), lakini hii haina maana ya kwamba hakuna masharti. Kuna haja ya kuwa na toba ya kweli, na pia kuna haja ya kuwa na imani ‘juu ya’ Yesu kuwa ndiye aliyelipa deni (ameibeba ile hukumu) ya dhambi. Tunaposema imani ‘juu ya’ katika sentensi,

tunakusudia kutilia umuhimu mkubwa, ambao sio tu wa kujengea mapendekezo ya kifikra kuhusu Yesu. Bali ni umuhimu unaohusu pia hali ya mtu binafsi kumuamini, na kujenga imani na kuwa muaminifu kwa Yesu, huku akiamini na kukiri ya kwamba sadaka aliyoitoa Yesu, kifo chake na ufufuo wake vyote vilikuwa ni kwaajili yako, ili kuondoa dhambi zako na kukuongoza katika njia yake. Toba ya kweli si tu kusema samahani. Inahusu pia hali ya kuacha matendo ya dhambi, kuacha tabia ya dhambi na kumgeukia Kristo! Toba ya kweli haitakuwepo wala haitawezekana kama nguvu zetu sisi wenyewe tutashindwa kusamehe. (Tazama Mathayo 6:12, 14, 15; 18:21-35; Luka 17:3-4. Tazama pia Warumi 3:24; 4:7; Waefeso 4:32; Wakolosai 2:13; 3:13; Matendo 10:43; 1 Yohana 1:7; 2:2. Hali ya kutowasamehe wengine itaadhibiwa (tazama tena Mathayo 18:21-35). Mungu, katika upendo wake wa kweli wa 'agape' yuko tayari na ana nia ya kumsamehe kabisa mwenye dhambi anayetubu. Hatimaye ni uamuzi wetu kuukubali ule msamaha uliotolewa ama kuukataa. Kumbuka ya kwamba, hii ndiyo siku ya wokovu' – kwahiyo ukisubiri kesho unaweza kuwa umekwisha kuchelewa. (tazama 2 Wakorintho 6:1-2)

Mawazo wa Mwisho

Kwakuwa ni Mungu mmoja tu wa kweli aliye mtakatifu, ni yeye tu ndiye anayeweza kusamehe dhambi. (Marko 2:7; Luka 5:21). Tunauona utakatifu wa kweli wa Yesu katika huduma yake ya hapa duniani aliposamehe dhambi. Kila dhambi hatimaye hupingana na Mungu (mfano Zaburi 51:4). Msamaha wa dhambi haupatikani kutoka kwa 'miungu' wengine, wala kutoka kwenye dini nyingine za ulimwengu zisizo Ukristo. Hata katika mawazo, kupitia mazungumzo katika dini hizo nyingine msamaha hauna maana inayofanana na ile iliyopo katika Ukristo. Kwa mfano, katika dini za jadi hakuna mahusiano ya kibinafsi (wala hali ya kujisikia kuwajibika) na Mungu wa kweli aliye hai. Dini ya Kihindi inadai ya kwamba kila mtu anapaswa kupitia mateso ikiwa ni sehemu ya matokea ya mzunguka wa maisha ya kuzaliwa kufa na kuzaliwa tena – lakini haitoi matumaini yoyote ya msamaha. Dini ya Ubudha haijui mungu yeyote anayesamehe. Katika Uislamu hakuna mahusiano yoyote ya kibinafsi na mungu (hakuna Baba wa mbinguni wala Mwokozi binafsi). Baadhi ya tofauti kati ya dini zimetolewa kwenye kitabu kiitwacho The Empty Promise of Godism ambacho kinapatikana bure na unaweza kukipakua kwenye tovuti ya – Glory to Glory – kwa lugha ya kiingereza - hasa sura ya 6.

Msamaha wa dhambi ni muhimu ili kuweza kuwa na faragha na Mungu – Baba, Mwana na Roho Mtakatifu (tazama hasa 1 Yohana 1:3 na 2 Wakorintho 13:14) Mtume Paulo mara kwa mara alitumia maneno, 'katika Kristo', na 'katika Bwana' (mara 164) jambo ambalo linatilia umuhimu ushirika na Mungu, na kuashiria ya kwamba ni watu ambao dhambi zao zimesamehewa. Msamaha upo katika kiini cha maisha na ujumbe wa Ukristo.

Copyright © Sovereign World Trust, PO Box 777, TONBRIDGE, Kent, TN11 0ZS, UK
www.sovereignworldtrust.org.uk

Publishing and Translation History

First Published in English by Glory to Glory Publications.

Christian Publications International, PO Box 212, Saffron Walden, CB10 2UU - www.christian-publications-int.com
Editor Peter Sammons. Contributors Alex Jacob, David M. Moore, Peter Byron-Davies, Greg Stevenson, Peter Sammons
ISBN English 978-0-9567831-6-5

This Kiswahili translation for Sovereign World Trust by Revd John Y Madinda with permission
Swahili Edition Published by Sovereign World Trust ISBN - Kiswahili 978-1-908010-12-4